

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOMBERO**

(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya)

Simu: 023 - 2931523

Fax: 023 - 2931513

E-mail : [ded@kilombero.go.tz](mailto:ded@kilombero.go.tz)

E-mail : [psded@kilombero.go.tz](mailto:psded@kilombero.go.tz)



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W),

S. L. P. 263,

**IFAKARA.**

**Unapajibu tafadhalii taja:**

Kumb.Na.KDC/L.10/3/VOL.IV/25

23/03/2018

**YAH: TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero anatangaza nafasi za kazi za Watendaji wa Vijiji Daraja la III kwa masharti ya kudumu. Tangazo hili ni baada ya kupokea kibali cha ajira mbadala chenye Kumb. Na. CFC 26/205/01 "F"/91 cha tarehe 22/08/2017, Pamoja na barua ya nyongeza ya muda wa utekelezaji kibali cha ajira mbadala kwa Watendaji wa Vijiji na Mitaa yenye Kumb Na. CFC.26/205/01 "GG"/95 ya tarehe 12,Machi, 2018 zote kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais (UTUMISHI).

Mchanganuo wa nafasi za kazi ni kama ifuatavyo:-

**1. MTENDAJI WA KIJIJI DARAJA LA III (NAFASI 50)**

**SIFA ZA MWOMBADI**

Awe na cheti cha kuhitimoo na kufaulu Kidato cha Nne (IV) au cha sita (VI) aliyehitimoo mafunzo ya Astashahada/Cheti katika moja ya fani zifuatazo:-

Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya sanaa kutoka chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

## **MAJUKUMU:**

- i. Afisa masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji
- ii. Kusimamia ulinzi na Usalama wa raia na mali zao, kuwa Mlinzi wa Amani na Usimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji.
- iii. Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji.
- iv. Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji.
- v. Kutafsiri na Kusimamia Sera, Sheria na Taratibu.
- vi. Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha Wananchi katika kuandaa na utekelezaji mikakati ya kuondoa njaa, umasikini na kuongeza uzalishaji mali.
- vii. Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya Kitaalam katika Kijiji.

## **NGAZI YA MSHAHARA**

Atalipwa mshahara katika ngazi ya TGS. B sawa na shilingi za kitanzania 390,000/= kwa mwezi.

## **MASHARTI YA JUMLA**

1. Mwombaji awe Raia wa Tanzania na awe tayari kufanya kazi sehemu yoyote kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero.
2. Mwombaji awe na umri kati ya miaka 18 na usiozidi miaka 45 na awe hajawahi kupatikana na kosa la jnai au kufungwa jela.
3. Maombi yote ya waombaji waambatanishe maelezo binafsi yanayijitosheleza (detailed CV) namba za simu na anuani sahihi.
4. Maombi yote ya mwombaji yaambatane na nakala za vyeti vya taaluma, vyeti ya Kidato cha (IV au VI), Chetia cha kuzaliwa na picha mbili (2) za passport size za hivi karibuni (Passport size na iandikwe jina kwa nyuma).
5. Testimonials na provisional statement of results hati ya matokeo ya kidato cha nne na sita **HAVITAKUBALIWA**.
6. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na mamlaka husika (TCU na NECTA) na taarifa ya uhakiki iambatanishwe kwenye maombi.

7. Siku ya usaili kila mwombaji afike na vyeti halisi vya Elimu, Taaluma, Kuzaliwa na Kitambulisho.
8. Waombaji waliostaafishwa au kuacha kazi katika utumishi wa Umma hawataruhusiwa kuomba isipokuwa kama wana kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.
9. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.
10. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 06 April 2018 saa 9:30 alasiri.
11. Barua zote ziandikwe kwa mkono wa mwombaji na kutumwa kwa anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi Mtendaji,  
 Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero,  
 S.L.P. 263,  
**KILOMBERO.**

**NB:** Masharti yaliyoainishwa kwenye tangazo hili yasomwe kwa makini na yazingatiwe.

Dennis Lazaro Londo  
**MKURUGENZI MTENDAJI (W),**  
**KILOMBERO.**

<b>MKURUGENZI MTENDAJI (W)</b>
<b>HALMASHAURI YA WILAYA</b>
<b>KILOMBERO</b>
<b>S. L. B. 263</b>
<b>IFAKARA</b>

**Nakala:** Katibu Tawala (M),  
 " Katibu Tawala (W),  
 " Mbao zote za Matangazo